

Kumbukumbu 22:5" Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako".



Na bado Isitoshe BWANA anawapelekea watu wake kuwaonya lakini bado wanadhihaki na kuziba masikio yako wasisikie

Warumi 1:18-28" Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu.

Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayo julikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia.

Kwa sababu mambo yake yasiyo onekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru; kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.

Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika;.....Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao. Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo,.....

Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili;

wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao. Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa.

Tunahitaji uthibitisho gani tena kuwa tunaishi katika siku za mwisho nyakati

za hatari kama hizi?? JE! umeokolewa,..umempa KRISTO maisha yako? umeoupokea ujumbe wa wakati huu aliouleta Mungu kuitia mjambe wake ndugu William Marrion Branham wa kanisa la saba na la mwisho ?.

Kama hujafanya hivyo ndugu ni vema ukamgeukia BWANA kabla mlango haujafungwa...

Mungu akubariki.

Pia unaweza ukapata mafundisho haya Kwa njia ya Whatsapp yako, jiunge na channel yetu Kwa kubofya hapa >> **WHATSAPP**

Kwa msaada wa maombi/Ushauri/ubatizo/mafundisho/Whatsapp: Namba zetu ni hizi:

+255693036618/ +255789001312

Jiunge na magroup yetu ya whatsapp kwa kubofya hapa > WhatsApp-Group

Mada Nyinginezo:

KIKOMBE CHA GHADHABU YA MUNGU KINAJAA.

SIKU YA HASIRA YA BWANA.

SIRI YA MUNGU.

JE! KUFANYA MASTURBATION (PUNYETO) NI DHAMBI?

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp